

WATENDAJI wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar wameishauri Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kusambaza watendaji wake kila taasisi za umma na binafsi ili kupata taarifa sahihi na kuibua mianya ya rushwa .

Wakizungumza navyombo vya habari baada ya kupatiwa elimu juu ya wajibu wa watumishi katika mapambano dhidi ya rushwa katika ukumbi wa video game kariakoo Unguja Wilaya ya Mjini.

Wamesema iwapo ZAECA itasambaza watendaji wake kila taasisi itasaidia kuibua na kudhibiti mianya ya rushwa na uhujumu wa uchumi na kupatikana kwa taarifa sahihi ambazo zitasaidia serikali kwa lengo la kuwepo kwa maendeleo endelevu nchini.

Akifunga kikao hicho kaimu meneja rasilimali watu na utawala Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar Ali Suleiman amewataka watendaji hao kufuata vyema sheria, kanuni na maadili ya kazi sambamba na kuchukua vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi ili kufikia lengo la serikali.

Afisa elimu wamamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar (ZAECA) Sada Salum Issa amesema lengo la elimu hiyo ni kuwahamasisha watumishi ili waweze kujiepusha na vitendo hivyo ambavyo vinaweza kufanyika bila ya kukusudia.